

# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

Octoba 2017

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika".

- Joseph Wresinski (1917-1988), founder of ATD Fourth World -



Tarehe 17 Oktoba  
Siku ya  
kuutokomeza  
umaskini  
uliokithiri duniani

Tahariri



Rafiki Mpandwa,

Tunafuraha kupendekeza kwako toleo maalum la jarida linaloelezea kuhusu siku ya kimataifa ya kuushinda umaskini uliokithiri tarehe 17 mwezi wa 10. Kama unavyofahamu mwaka huu tutaadhimisha maadhimisho ya miaka 30 ya siku hii lakini si hivyo tu. Katika muundo wa wito wa kampeni ya kuchukua hatua, pia tutasherehekea maadhimisho ya miaka 100 ya Joseph Wresinski na miaka 60 ya shirika letu. Tukifuata muendelezo uleule wa mara ya kwanza.

Katika mwaka huu mzima sisi wanakamati wa Kamati ya Maandalizi ya Oktoba 17 tumekuwa tukiandaa tukio hili kulifanya kuwa fursa kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri waweze kusikika katika jamii. Tilitaka kuwashirikisha kwa upana wanachama wetu hai na kuwashakikisha ushiriki na uwepo wa kila mmoja. Maadhimisho ya pekee yanaratibiwa kwa ajili ya **tarehe 14 mwezi Oktoba 2017 jijini Dar es Salaam**.

Katika ukurasa wa 3 utaweza kusoma hutuba ya Joseph Wrisinski ya "ninatoa ushuhuda kwako" aliyoitoa tarehe 17 Oktoba mwaka 1957 katika uwanja wa Haki za binadamu jiji Parisi Ufaransa. Tukifuata moyo huo tumpanga utaratibu utakaunganisha sauti zetu na za wale wanaoishi katika ufukara, wakipambana kila siku kukabiliana na mazingira yao. Kama unavyofahamu mwaka huu Shirika la ATD Dunia ya Nne limeratibu kampeni inayoitwa **UMASKINI BASI**, iliyozinduliwa rasmi tarehe 12 Februari 2017. Kampeni hii inalenga kukusanya idadi ya watu wanaotaka kutokomeza umaskini uliokithiri duniani kote. hii ni namna ya kuonesha mshikamano wetu pamoja na watu wanaopigana dhidi ya umaskini uliokithiri.

Katika ukurasa wa mwisho tunakukaribisha kusoma tafakari za vijana, mustakabali wa jamii yetu. Ujumbe wa vijana wanne kutoka katika kikundi cha vijana amba ni Agatha, Halfani, Pazi na Vicky amba walikwenda Bukavu Congo kushiriki katika semina iliyohusu Elimu kwa Amani. Walishirikishana fursa walizokuwa nazo kugundua kujitolea kwao. Kama Vicky alivyosema, "ushirikiano kutoka katika makundi ya matabaka mbalimbali unaleta amani kwa sababu katika umoja tunaonekana kuwa wamoja."

Tunawataki marafiki wote kila mahali Tanzania na kote duniani mafanikio na furaha katika siku ya Oktoba 17.

Sisi Kamati ya Maandalizi ya Oktoba 17. ATD Dunia ya Nne Tanzania TAHARIRI JARIDA LA OCTOBA 2017

**"Tunapoishi na mkusanyiko kama huu kwa pamoja kunakitu tunajenga." Rehema Abdallah (Tandale, Dar es Salaam)**

Nakumbuka siku moja niliambiwa kwamba kuna siku ya kutokomeza umaskini Oktoba 17. Niliambiwa kwamba sherehe zitafanyikia viwanja nya Mnazi Mmoja. Sherehe hiyo ilikuwa kubwa na ilihudhuriwa na mashirika mbalimbali, ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kusikia kuhusu Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Umaskini watu wanakutana kusherehekeea kwa pamoja. Nilipokwenda nilisikia shuhuda mbalimbali watu walizotoa, hapo ndipo nilipofahamu ahaa! kuna njia ya kupambana na umaskini bila ya kumpa mtu fedha, shuhuda hizo zinaweza kukusaidia kugundua na kutambua kwa kina njia nydingine zinazoweza kukusaidia. Ukifuata njia kama hiyo unaweza kuushinda umaskini

Kila mwaka sherehe zinakuwa tofauti, wakati mwininge zinakuwa kubwa kama ile iliyofanyika Mnazi Mmoja, na wakati mwininge inakuwa ndogo kama ile iliyofanyikia Tegeta au ile iliyofanyikia katika Kijiji cha Makumbusho Ninapendelea sherehe ndogo, sherehe ikiwa ndogo unapata fursa ya kubadilishana mawazo na watu. Siku hii ni muhimu sana kwa sababu unajifunza mambo mengi kutoka sehemu nydingine. Nina uzoefu na umaskini katika maeneo yangu lakini ninaposhiriki katika tukio kama la Oktoba 17 ninajifunza zaidi. Unapokuwa peke yako katika maeneo yako unaweza kufikiri wewe ndio maskini wa kutupwa, lakini unapohudhuria katika maadhisho ya tarehe 17 Oktoba unagundua kuwa kuna maskini zaidi yako. Siku hii ina maana kubwa sana kwa sababu nasikiliza changamoto za watu wengine na wao kusikiliza changamoto zangu kwa sababu mimi sifichagi nawaambiaga mimi mwenyewe nipo katika hilo kundi. Sasa, ninapokutana na watu, nawauliza kama walishawahidi kusikia kuhusu Oktoba 17, kama hawajawahi kusikia nawafahamisha. Siku ya tarehe 17 mwezi wa kumi duniani kote watu wanaadhishira siku hii, sherehe kama hii hajulikani sana hapa, ni watu wache tu wanafamu. Nawafahamisha watu kwamba ni wakati watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanakusanyika kwa pamoja na kupaza sauti zao kwa pamoja na kusikilizwa na watu. Kwa sababu kwa kawaida sauti za maskini hazisikilizwi.

Ni muhimu sana kwa watu kusanyika katika siku kama hii kwa sababu tunaishi katika matabaka, na kutengana. Tunapokuwa kwenye mkusanyiko kama huu kwa pamoja kuna kitu kitajengeka. Kisha wote tutagundua kwamaba watu wote ni sawa, watu wasioishi katika umaskini watagundua juhudhi za watu wanaoishi katika umaskini wanavyo pambana dhidi ya kutengwa, watagundua changamoto wanazo kabiliana nazo. Watu wanaoishi katika umaskinini wakizungumza na watu wengine wakisikiliza mabadiliko yanakuja. Siku ya tare kumi na Saba mwezi wa Kumi ingekuwa vizuri kama kungekuwa na wawakilishi kutoka serikalini wakisikiliza shuhuda kwa sababu watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri hawawezi kufikisha sauti zao wenye kati ngazi za juu serikalini. Kama mawakili, wangeweza kusikiliza na kuzifanya kazi katika ngazi ya serikali.



<http://urlz.fr/5r2k>

Toa sauti yako ,acha usuhuda wako. Uliza wanaokuzunguka wanachama wengine wa ATD Dunia ya Nne, shirkiana na familia yako, marafiki, majirani kujunga na wito wa kuchukua hatua.

**STOP  
POVERTY**  
ALL TOGETHER IN DIGNITY

## 2017 Wito kwa Kampeni ya kuchukua Hatua

Saini na ungana na maelfu ya watu

**Wasanii wanahamasisha  
katika kuadhimisha miaka  
thelathini ya siku ya  
kimataifa ya kuushinda  
Umaskini Uliokithiri**



Husein Omari Munju na Violet Nahum Malle ni wanachama wa Kundi la elegant, kikundi cha wasanii watakoahamasisha katika maadhisho ya siku ya Kimataifa ya Kuukataa Umaskini, tarehe 14 Oktoba 2017 jijini Dar es Salaam. Kwa muda wa miezi kadhaa, Husein Omari Munju na Violet Nahum Malle wamekuwa wakiandaa siku hii pamoja na Kamati ya Maandalizi ya siku hii. Munju ameandaa burudani ya siku nzima itakayojumuisha nyimbo, ngojera na igizo. Violet ataimba, atacheza na atashirikiana kutumbuiza na wanakikundi wenzake.

Munju aligundua maadhisho haya katika Kijiji cha Makumbusho mwaka jana na alivutiwa sana na uhamasishaji wa watu kuukataa udhalimu. Munju alisema: "Oktoba 17 ni siku yangu kwa sababu nami pia niliupitia. Siku hii itaonesha kwamba tunaweza kutengeneza chochote kama raia wa Tanzania."

Violet alisema kwamba tarehe 17 Oktoba ni siku maalum ambayo hata watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanaweza kuungana na wengine kusaidiana katika kupaza sauti zao ili waweze kusikika kwa watanzania wote na pia katika ulimwengu mzima.

## Wapi?

Viwanja nya Biafra, Barabara ya Morocco, Kati ya Manyanya na Kituo cha Mwendo kasi Morocco – Kituo cha daladala Kanisani Dar es Salaam Tanzania

## Lini?

**Tarehe 14 Oktoba**  
**Kuanzia saa tatu hadi saa**  
**sita mchana**

- ✓ Shuhuda mbalimbali zinaohusiana na watu wanaoishi katika umaskini wanavyo pambambana na umaskini.
- ✓ Maigizo, yanaohusiana na harakati za kupambana na umaskini
- ✓ Ujumbe kutoka sethemu mbalimbali za dunia, kama vile Umoja wa Mataifa, Ujumbe kutoka makao makuu ya shirika la ATD Dunia ya Nne
- ✓ Siku hii itapambwa na wito wa kuchukua hatua kwa vitendo kwa kuunga mkono kampeni ya umaskini basi kwa kusaini ili tupate idadi kubwa ya watu wanabunga mkono umaskini basi.
- ✓ Kutakuwa na burudani mbalimbali.

## Miaka thelathini ya siku ya kimataifa ya kuushinda Umaskini Uliokithiri

**Tarehe 14 Oktoba, 2017, Dar es Salaam**

Joseph Wresinski,  
Mwasisi wa ATD Dunia ya Nne (1917-1988)



Mnamo tarehe 17 Oktoba 1987, idadi ya watu 100,000, watetezi wa haki za binadamu, walikusanyika pamoja katika Uwanja wa Haki za Binadamu jijini Paris kutoa heshima kwa wahanga wa wa njaa, vurugu na ujinga. Joseph Wresinski alitoa hotuba yake maarufu "Ninatoa Ushuhuda" akionesha siyo tu mateso, bali ujasiri, juhudhi na matamanio ya hao wanaoishi katika umaskini uliokithiri ulimwenguni kote.

### Ninatoa ushuhuda kwenu,

Ninyi mamilioni kwa mamilioni ya watoto, akina mama kwa akina baba walifariki kwa ufukara na njaa, tuliowarithi. Ninyi mliokuwa hai, siyo kifo chenu ninachokitambulisha leo kwenye Uwanja huu wa Fadhila, wa Haki za binadamu na Raia bali ni maisha yenu ninayoyashuhudia.

Nawashuhudia ninyi, akina mama mnaona watoto wenu wanahukumiwa kuishi katika ufukara, wakawa kama mali ya ziada duniani humu. Nashuhudia watoto wenu wenye mwili ulionyong'onyea kwa mateso ya njaa waliopoteza tabasamu bado wangalitaka kupenda. Nashuhudia mamilioni ya Vijana waliopoteza sababu zao za kusadiki wala za kuwepo duniani, wakitarajia bure siku za usoni duniani humu kusiko na maana.

Nawashuhudia maskini wa nyakati zote na tena wa leo wanaovutwa na safari wakakimbia huku na kuko kati ya dhara na chuki. Wafanyakazi, wasio na fani, wanaotingwa muda wote na kibarua, wafanyakazi ambao mikono yao sasa, haina faida tena.

Mamilioni ya wanaume wanawake na watoto ambao miyo yao bado hupiga mapigo makubwa ya kujitahidi, Akili zinaasi dhidi ya majaliwa yasiyo na haki walikandamizwa wenye ushupavu unaodai haki ya kuthaminika zadi.

Nawashuhudia ninyi watoto; wanawake kwa wanaume Mnaokataa kulaani, bali kupenda kusali, kufanya kazi na kushirikiana ili izaliwe ardhi yenye ushirikiano, ardhi moja, ardhi yetu, ambapo kila mtu angaliweka ndani yake wema wake uliobora kabla ajafa.

Nawashuhudia wanaume, wanawake na watoto Ambao sifa yenu imeishachongwa kwa moyo, mkono na chombo katika jiwe la Uwanja huu wa Fadhila. Nawashuhudia ili watu, mwisho wajiongoze katika busara wakakatalia kwa daima kule kuwa fukara hakuwezi kuepukwa.



**Kuoka** tarehe 2-8 July 2017, baadhi ya vijana walikwenda Congo kuiwakilisha ATD Dunia ya Nne kwenye semina iliyokuwa inahusu namna ya kudumisha Amani katika jamii zetu. Kundi la vijana walipendekeza watu wa wanne ambaa ni Khalfani, Vicky, Pazi kutoka maeneo ya Tandale na Agatha kutoka Magomeni. Kundi la vijana la ATD hapa Tanzania liliwahi kupata nafasi ya kukutana na marafiki kutoka Bukavu Congo kwenye semina iliyokuwa na Ujumbe namna tunavyoweza kuwa marafiki kwa wasiokuwa na marafiki iliyofanyika Dar es Salaam Mwaka 2016. Wakati huu ilikuwa ni nafasi ya Marafiki zetu wa Congo kuwaalika marafiki wa Tanzania. Ni namna gani vijana walipata uzoefu kuititia safari kwa masiku waliyokaa na kushiriki kwenye Mikutano, kwa yale waliyofunza na kugundua yanaweza kutufanya kuelewa kwa kina zaidi nini hasa maana ya urafiki katika kupambana na umaskini uliokithiri.

**Pazi:** Kwa mimi kilichonigusa na kunisisimua ni namna marafiki wa ATD Dunia ya Nne Congo wanavyokuwa karibu na watu wanaoishi katika makazi duni sana. Hali hii imenifanya kutambua kwamba ni jukumu letu kuwaafuata wale wote walioachwa nyuma na kuwa karibu nao. Niliona milima mingi midogodogo wale wengi walioachwa nyuma na kusahaulika ndio wanaoishi huku.

**Khalfani:** Watu wanaishi kwa kushirikiana siku hadi siku, watu ambaa si maskini na wanaoishi kwenye umaskini wanakuwa kitu kimoja. Huzitembelea mara kwa mara familia maskini, marafiki na watu kutoka kwenye jamii huwasaidia walio maskini kukarabati nyumba zao. Na pia kwenye kipindi cha maktaba ya mtaa watoto hupewa nafasi ya kuonesha vipaji vyao kama vile kuimba, kucheza hivi ni vitu vinavyopewa mkazo sana.

**Vicky:** Nimeguswa na namna wanavyopangilia shughuli zao, kama vile jinsi wanavyogawana majukumu kama vijana. Niliposhiriki Maktaba pamoja nao kila mmoja alikuwa akitimiza majukumu yake kwa umakini wa hali ya juu. Maktaba ya mtaa kwa wao ni sehemu ya kila mmoja kuonesha kile anachowesta kufanya bali si sehemu tu ya wawezeshaji ni sehemu pia ya watoto.

## Kikundi cha Vijana Bukavu, Kongo. Tujenge amani katika jumuia yetu

**Pazi:** Semina ya Umuseke ilihushwa na kujenga amani katika jumuia zetu. Kitu kimoja nilichojifunza ni kwamba inatubidi kufanya utafiti kabla ya kuchukua maamuzi kwa vitu tulivjosikia au kuona. Ni muhimu sana kudumisha amani lakini kuna masuala mengi yanayoweza kuiondoa. Wakati mwengine tunahukumu wengine kwa sababu wanaonekana kuwa tofauti, wana tabia zisizo za kawaida. Tunaweka watu katika makundi na hatutambui kwamba wanaweza kuwa muhimu kama wengine, mambo kama haya yanaweza kuondoa amani.

**Vicky:** Ushirikiano kutoka kwa watu wenye matabaka tofauti hupelekea kuleta Amani kwasababu muungano hujenga hali ya umoja. Umoja hujenga ile hali ya kuweza kubadilishana uzoefu na huepusha ile dhana ya kujenga matabaka. Ushirikiano husaidia kwenda mbele zaidi na ndani yake pia huimarisha amani. Pindi Amani inapoimarika husaidia watu kuwa watulivu na kuweza kutatua changamoto za kila siku.

**Pazi:** Kwa mtazamo wangu, naona inatupasa kuwa karibu na wale watu walioachwa, kwa kuendelea kuwa nao inatuhamasisha zaidi kuendelea kujitoa.

**Khalfani:** Mikutano husaidia kugundua mawazo tofauti, kupata uzoefu tofauti na kuongeza ujuzi kutoka kwa marafiki wengine katika harakati kuititia ile ambayo watu wanapaza sauti zao kuukata umaskini uliokithiri.

**Agatha:** Kuititia mikutano, kubadilishana uzoefu wakati tupo Congo, Imenitia nguvu zaidi ya kuendelea mbele ili kuweza kujengwa Dunia amabayo itakuwa na usawa kwa kila mmoja na hii pia ni nafasi kwangu kuwatia nguvu wengine wanaonizunguka. Kuwa na marafiki ni muhimu kwasababu kuwa na marafiki unaweza kujifunza, kugundua yalo mengi kwa kusikiliza au kuona husaidia pia kupanua taaluma kutoka kwa watu wengine.



Wasiliana nasi!